**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**686** **VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu 05 Mei, 2003**

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **40** na sehemu **B** na **C** zina alama **30** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

1. Orodhesha zana nne atakazotumia mwalimu kumfundisha mtoto stadi ya kusimulia.

2. Chambua kwa kifupi changamoto nne za kutumia mbinu ya igizo katika kufundisha hatua za ukuaji wa lugha kwa mtoto.

3. Bainisha njia nne anazoweza kuzitumia mtoto ili kuweza kutambua maneno katika kujifunza lugha.

4. Taja mazoezi manne ya kulainisha viungo vya mtoto ili kumwandaa kujifunza stadi za awali za kuandika.

5. Eleza kwa kifupi jinsi mtoto anavyoweza kutumia lugha katika kujenga mahusiano mazuri katika jamii.

6. Fafanua kwa kifupi matendo manne ambayo mzazi anaweza kuyafanya ili kukuza lugha kwa mtoto wa miaka sifuri hadi miwili.

7. Onesha hatua nne za kufuata wakati wa kufundisha kuandika herufi 'b'.

8. Orodhesha zana nne ambazo mwalimu anaweza kutumia kumfundisha mtoto kutamka maneno.

9. Fafanua kwa kifupi jinsi mazingira yafuatayo yanavyochangia katika kujifunza stadi za awali za kusoma kwa mtoto:

   (a) Mazingira ya nyumbani

   (b) Mazingira ya shuleni

10. "Mbinu za kufundishia stadi ya kuandika kwa watoto wa darasa la awali lazima ziwe na Sifa stahiki." Ainisha sifa nne.

## SEHEMU B (Alama 30)

11. "Mwalimu anapomfundisha mtoto stadi za awali za kuzungumza anaweza kukutana na changamoto nyingi." Thibitisha kauli hiyo kwa hoja tano.

12. Kwa kutumia mifano, eleza manufaa anayoyapata mtoto katika ujifunzaji wa lugha. Tumia hoja tano.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

13. Kwa kutumia mfano kwa kila moja, fafanua hatua tano za kufuata katika ufundishaji wa kuandika herufi za Kiswahili katika Darasa la Awali.

**SEHEMU C (Alama 30)**

14. Ili kuepuka changamoto zinazoweza kujitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu hama bade kufanyia majaribio zana za kufundishia na kujifunzia kabla ya kuingia darasani. Chambua faida sita za kufanyia majaribio zana za kufundishia na kujifunzia stadi ya kuandika.

15. Chambua kwa kina hatua tano utakazozifuata unapomfundisha mtoto kusoma neno "baba" kwa kutumia mbinu ya onesho.

16. Bainisha matendo matano atakayoyafanya mwalimu kumzofisha mtoto kusikiliza kwa makini.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org